

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTHARA – MIKINDANI

TANGAZO LA MAOMBI YA MIKOPO

**MKURUGENZI WA MANISPAA ANAWAALIKA VIKUNDI VYOTE VYA
KIUCHUMI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE
ULEMAVU VYENYE SIFA ZILIZOORODHESHA HAPO CHINI
KUOMBA MKOPO**

UTARATIBU NA MASHARTI YA UOMBAJI WA MIKOPO KWA VIKUNDI

- I. Kikundi kimesajiliwa kama kikundi cha wanawake, vijana au watu wenye ulemavu
- II. Kikundi hakitajumuisha wajumbe wenye ajira rasmi.
- III. Kikundi kinajishughulisha na ujasiriamali (Shughuli ya Pamoja)**
- IV. Kwa kikundi cha wanawake au vijana kina idadi ya wanakikundi kuanzia kumi (10) na kuendelea na kwa kikundi cha watu wenye ulemavu, kina idadi ya wanakikundi isiyopungua watano (05) na isiyozidi kumi (10);
- V. Kina akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya kikundi;
- VI. Wanakikundi wake ni raia wa Tanzania wenye akili timamu na umri wa miaka kumi na nane na kuendelea;
- VII. Kwa vikundi vya vijana wanavikundi wawe na umri kuanzia miaka **18** na usiozidi miaka **35**
- VIII. Kikundi kinachokusudia kuomba mkopo kitatakiwa kujaza fomu zinazopatikana katika ofisi za kata kupitia Afisa maendeleo ya jamii wa kata husika

IX. Kikundi kitakaporejsha fomu ya maombi ya mikopo kinatakiwa kurejesha nakala za nyaraka zifuatazo

(a) Nakala za nyaraka zifuatazo:

- (i) katiba ya kikundi;
- (ii) cheti cha usajili wa kikundi
- (iii) Kwa vikundi vinavyojishughulisha na biashara, leseni ya biashara
- (iv) Cheti cha kuzaliwa au kitambulisho cha taifa kwa vikundi vya vijana

(b) Nakala halisi za nyaraka zifuatazo:


- (i) Taarifa ya akaunti kutoka katika benki ambayo kikundi kina akaunti;
- (ii) Barua ya utambulisho kutoka kwa Mtendaji wa Kata
- (iii) Wazo la biashara

Fomu zitaanza kutolewa katika Ofisi za Kata kuanzia tarehe **03 Februari 2020**

Mwisho wa kurejesha fomu za maombi ya inkopo ni tarehe **21 Februari 2020**

Fomu zote zilizokamilika ziwasilishwe katika ofisi ya Kata kwa Afisa Maendeleo ya Jamii wa Kata husika

Imetolewa na;



**MKURUGENZI WA MANISPAA
MTWARA MIKINDANI**